JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 123,
Simu: (023) 2334013,
Nukushi: (023) 2333726
Barua pepe: rbcmtwara@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

**MEI, 2022**

# TAKUKURU MTWARA YAFUATILIA UTEKELEZAJI WA MIRADI 38 YA ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 10.

## UTANGULIZI:

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Nimewaita hapa kwa lengo la kuujulisha umma juu ya utendaji kazi wa TAKUKURU Mkoa wa Mtwara kwa kipindi cha **Januari, 2022 hadi Machi, 2022.** Utaratibu huu ni wa kawaida ambao TAKUKURU imejiwekea ili kuhakikisha kuwa umma wa Watanzania pamoja na wakazi wa mkoa wa Mtwara wanafahamu jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuzuia na kupambana na rushwa.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

## UCHUNGUZI:

Katika kipindi cha **Januari, 2022 hadi Machi, 2022,** Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mtwara iliendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kama yalivyotamkwa katika kifungu cha 7 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura ya 329 iliyorejewa mwaka 2019.

Katika kipindi tajwa jumla ya **malalamiko (45)** yalipokelewa TAKUKURU (M) Mtwara. Kati ya malalamiko **hayo 45, malalamiko 33** yalihusu rushwa na **malalamiko 12** hayakuhusu rushwa. **Malalamiko 33** yaliyohusu rushwa yanafanyiwa uchunguzi ili kuthibitisha makosa ya rushwa ambapo kati yake, malalamiko matatu uchunguzi wake umekamilika. Kwa **Malalamiko 12** ambayo hayakuhusu rushwa, **malalamiko 9** wahusika walishauriwa na kuelimishwa na **Malalamiko 3** yalihamishiwa idara nyingine.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**
**UENDESHAJI WA MASHTAKA:**
Katika kipindi cha **Januari 2022 hadi Machi 2022,** kesi **sita (6)** ziliendelea mahakamani na hakuna kesi iliyotolewa maamuzi. Katika kipindi tajwa kesi mpya mbili (2) zilifunguliwa.

**Ndugu Waandishi wa Habari.**

**UZUIAJI RUSHWA:**

Katika kipindi tajwa, ili kuzuia Rushwa, tumefuatilia matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa **Miradi ya Maendeleo 38** yenye thamani ya **shilingi 10,974,170,000.55** inayotekelezwa hapa mkoani Mtwara.

Katika miradi hiyo, miradi 6 yenye thamani ya shilingi 1,732,135,011 ilikuwa na kasoro. Kasoro zilizojitokeza ni pamoja na kutokupimwa kwa ubora wa vifaa (material test), kutokuweka jamvi la zege kwenye eneo lote la msingi wa majengo ya madarasa na ucheleweshaji wa ukamilishaji mradi kwa mujibu wa mkataba. Hatua zilizochukuliwa na TAKUKURU (M) wa Mtwara ni pamoja na uelimishaji umma juu ya umuhimu wa kusimamia miradi ya maendeleo na kushauri uboreshaji wa maeneo yaliyobainika kuwa na dosari. Aidha, miradi 32 yenye thamani ya shilingi 9,242,034,989.55 haikuwa na kasoro katika kipindi cha ufuatiliaji huu.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**
**UCHAMBUZI WA MFUMO:**

Katika kipindi cha mwezi Januari, 2022 hadi Machi, 2022 TAKUKURU(M) Mtwara ulifanya **uchambuzi wa mfumo** katika maeneo matatu (3) ambayo ni:- Tathmini ya utendaji kazi wa TEMESA mkoa wa Mtwara, uendeshaji mitihani vyuo vya elimu ya kati na tathmini ya utendaji kazi GPSA mkoa wa Mtwara**.**

**Malengo ya chambuzi** hizi ni kuainisha mafanikio, changamoto, fursa za uboreshaji ,kuainisha viatarishi vya rushwa katika utoaji wa huduma husika. Baada ya chambuzi hizi kukamilika matokeo yake hujadiliwa na wadau na kuweka mapendekezo ya namna bora ya kuziba mianya ya rushwa ili kuboresha huduma.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**
**UELIMISHAJI UMMA:**

Katika kuhakikisha kuwa TAKUKURU (M) wa Mtwara inashirikisha umma katika mapambano dhidi ya Rushwa, shughuli za kuelimisha Umma katika kipindi tajwa zilifanyika kwa kuendesha Semina **7**, mikutano ya hadhara **33**, kuimarisha Klabu **37** za wapinga rushwa katika shule za msingi, Sekondari na vyuo, Uandishi wa makala **3**, kuafanya maonesho **3,** Kuelimisha kupitia kipindi cha redio **1** na kutoa taarifa **1** kwa umma kupitia vyombo vya habari. Aidha jumla ya machapisho **2,102** yenye elimu dhidi ya rushwa yaligawiwa kwa wananchi.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**
**TAKUKURU INAYOTEMBEA:**

Pia kupitia TAKUKURU INAYOTEMBEA, kwa maana ya ofisi kuwafuata wananchi katika mahali walipo,TAKUKURU (M) wa Mtwara iliwatembelea wananchi katika maeneo ambayo miradi inatekelezwa kwa lengo la kukagua miradi, kutatua kero na kutoa elimu. Katika ziara hizi, elimu ilitolewa juu ya umuhimu na majukumu ya kamati za ujenzi, manunuzi na mapokezi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**
**TAKUSKA:**

TAKUSKA ni ushirikiano wa TAKUKURU na chama cha SKAUTI kwa lengo la kushirikisha vijana wa skauti katika mapambano dhidi ya Rushwa kwa kuwapa mafunzo kwani ni kundi muhimu sana. Tunaamini tukishirikiana nao pamoja na klabu za wapinga rushwa mashuleni na vyuoni tutapiga hatua kubwa zaidi katika kulea vijana wazalendo na wenye hari na uwezo wa kupambana na rushwa. TAKUKURU (M) Mtwara imetoa mafunzo kwa skauti ili kushiriki katika maonesho kwenye mabanda ya kuzuia rushwa wakiambatana na klabu za wapinga rushwa katika mbio za mwenge wa uhuru mwaka 2022.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**
**MIKAKATI YA APRILI – JUNI 2022:**

Katika kipindi kilichoanza **Aprili 2022 hadi Juni 2022**, mikakati ya TAKUKURU mkoa wa Mtwara katika kuzuia na kupambana na rushwa ni pamoja na ifuatayo:-

- Kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na mabaraza ya madiwani kwa lengo la kuwafanya wananchi kuchukua hatua na kushiriki katika uzuiaji wa Rushwa na kuacha kuwa walalamikaji tu.

- Kuendelea kutekeleza Mpango Kazi wa ushirikiano kati ya TAKUKURU na Chama cha SKAUTI - TAKUSKA

- Kuendelea kufuatilia matumizi ya fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi katika sekta za kimkakati za maji, afya, elimu na ujenzi (barabara).

- Kuendelea kufanya chambuzi za mifumo ili kubaini sababu zinazosababisha kuwepo kwa Rushwa na kutoa ushauri wa namna ya kurekebisha au kuboresha na hatimaye kutoa huduma bora.

**SHUKRANI NA WITO:**

TAKUKURU (M) wa Mtwara inapenda kuwashukuru wananchi na wadau wote wa mkoa wa Mtwara kwa ushirikiano wanaotupatia katika shughuli zetu na tunaomba tuendelee na moyo huu wa kizalendo. Pia napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Ndugu waandishi wa habari kwa ushirikiano wenu na pia nizidi kuwaomba kutuunga mkono katika kutekeleza majukumu yetu kwa kutupatia fursa katika vyombo vyenu ili kuwaelimisha wananchi kuhusu athari na madhara ya rushwa na namna salama na rahisi ya kukabiliana nayo. Natoa wito kwa kila mmoja wetu kwa nafasi yake kuzuia rushwa kwani kuzuia rushwa ni jukumu letu sote.

Imetolewa na:

ENOCK P. NGAILO
**MKUU WA TAKUKURU (M) MTWARA**
**0738150156**